JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI

WAKALA WA UFUNDI NA UMEME TANZANIA
(TEMESA)

MKATABA WA HUDUMA KWA MTEJA

SEPTEMBA, 2023

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UJENZI

WAKALA WA UFUNDI NA UMEME TANZANIA (TEMESA)

MKATABA WA HUDUMA KWA MTEJA

SEPTEMBA, 2023

YALIYOMO

DIBAJI iii
1.0 DIRA, DHIMA, NA MAADILI YA TAASISI. 1
1.1 DIRA 1
1.2 DHIMA 1
1.3 MAADILI YETU 1
2.0 MADHUMUNI YA MKATABA 2
3.0 WATEJA WETU 3
4.0 HUDUMA ZETU 3
5.0 VIWANGO VYA HUDUMA ZETU 5
6.0 WAJIBU WA WAKALA KWA MTEJA 18
7.0 HAKI NA WAJIBU WA MTEJA 19
7.1 *Haki za Mteja* 19
7.2 Wajibu wa mteja 20
8.0 MREJESHO WA UTOAJI WA HUDUMA 20
9.0 MAWASILIANO NA TAASISI 21

DIBAJI

Wakala wa Ufundi na Umeme (The Tanzania Electrical, Mechanical and Electronics Services Agency – TEMESA) ulianzishwa kwa Sheria ya Wakala Na. 30 ya mwaka 1997 ambayo inalenga katika utekelezaji wa mpango wa Serikali wa kuboresha utoaji huduma kwa Umma katika Wizara za Serikali na Taasisi zake. Kwa kupitia mpango huu TEMESA ilianzishwa tarehe 26 Agosti, 2005 kwa tangazo la Gazeti la Serikali Na. 254 la tarehe hiyo. Aidha, TEMESA ilizinduliwa rasmi tarehe 23 Juni, 2006. TEMESA ilikasimishwa karibu majukumu yote yaliyokuwa yanatekelezwa na Idara ya Ufundi na Umeme chini ya Wizara ya Miundombinu kwa malengo ya kutoa huduma bora na kwa ufanisi katika nyanja za Uhandisi Mitambo, Umeme, Elektroniki na Uendeshaji wa Vivuko.

TEMESA imeandaa Mkataba wa Huduma kwa Mteja kwa nia ya kuweka bayana huduma inazotoa na viwango vya huduma ambavyo wateja wa Wakala wanayo haki ya kuvitarajia; kuweka utaratibu wa kupokea maoni utakaowezesha kutambua namna wateja wanavyouona katika utoaji huduma zake, na utaratibu wa kupokea na kushughulikia malalamiko iwapo yatajitokeza. Wakala unaahidi kutoa taarifa ya utendaji kazi na utekelezaji wake kila mwaka kulingana na mkataba huu.

Aidha, Wakala utaendelea kuuboresha mkataba huu kuendana na mahitaji ya utoaji huduma yanayozingatia mabadiliko ya kiuchumi, kijamii, na kiteknolojia. Mkataba huu wa Huduma kwa Mteja utakuwa ni makubaliano ya kimaandishi kati ya TEMESA na wateja wake. Ili kufikia azma hii, Wakala umeweka bayana namna ya kupata mrejesho kutoka kwa wateja kwa njia ya pongezi, maoni, ushauri na malalamiko yenye nia ya kutoa mwongozo kwa watendaji wa Wakala kurekebisha ipasavyo utendaji katika utoaji wa huduma bora ili kukidhi matarajio ya walengwa.

Viwango vya huduma vimewekwa kwa kuzingatia maoni ya wateja, hali ya soko, mabadiliko ya teknolojia na uwezo wa Wakala kwa ujumla wake katika kutoa huduma hizo. Mkataba huu wa Huduma kwa Mteja, umelenga kuweka wazi haki na wajibu wa mteja na Wakala. Ili Mkataba huu uweze kutumika kwa mafanikio, ni lazima uwe mkataba hai ambao utafanyiwa mapitio kila baada ya miaka 5 au pungufu kulingana na mahitaji yatakayozingatia matokeo ya utoaji huduma na mrejesho wa wateja wetu kwa ujumla wao.

Mwisho, napenda kurasimisha matarajio yangu kuwa mkataba huu utakuwa kiungo rahisishi cha uhusiano wetu na wale tunaowahudumia. Hivyo, naridhia matumizi yake nikiimanika

kuwa wateja wetu watautumia na kutupatia mwitiko stahiki ili kuchochea maboresho ya huduma tutoazo.

Lazaro N. Kilahala
MTENDAJI MKUU

1.0 DIRA, DHIMA, NA MAADILI YA TAASISI.

1.1 DIRA

Kuwa Taasisi yenye ufanisi na ubunifu inayotoa huduma za kihandisi Tanzania bara kwa ajili ya kumridhisha mteja.

1.2 DHIMA

Kutoa huduma za uhakika, salama na zenye ubora wa hali ya juu katika fani ya uhandisi Mitambo, Umeme na Elektroniki, huduma za Vivuko na ukodishaji Mitambo kwa kutumia teknolojia ya kisasa.

1.3 MAADILI YETU

i. **Uadilifu**

Tunafanya kazi kwa uamifu na ukweli kwa wateja wetu;

ii. **Utendaji kazi wa pamoja**

Tunafanya kazi kwa pamoja na kushirikiana miongoni mwa watumishi ili kufikia malengo yaliyokusudiwa;

iii. Uweledi

Tunahakikisha tunazingatia utaalam na kufanya kazi kwa weledi wa hali juu;

iv. Uwajibikaji

Tunajituma katika utendaji kazi na kutimiza matakwa ya wateja na taifa kwa ujumla

v. Uwazi

Tunafanya kazi kwa uwazi na kuwa tayari kukaguliwa katika masuala ya kifedha na kiutendaji

2.0 MADHUMUNI YA MKATABA

Madhumuni ya Mkataba huu ni kuufahamisha umma juu ya aina na viwango vya ubora wa huduma tunazotoa. Kuwajulisha wateja haki na wajibu wao katika huduma zitolewazo na Wakala. Aidha, Mkataba unalenga kuboresha utoaji wahuduma kwa wateja wetu na umma kwa ujumla na kuongeza uwajibikaji wetu katika kuwahudumia kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa. Mkataba umeweka wazi utaratibu wa kutoa mrejesho utakaowezesha Wakala kuboresha huduma ili kukidhi mahitaji na matarajio ya wateja.

3.0 WATEJA WETU

Katika Mkataba huu tunatambua Wateja wetu kama ifuatavyo:

i. Taasisi za Umma;

ii. Mashirika yasiyo ya kiserikali;

iii. Wafadhili na Wahisani;

iv. Mashirika ya Kimataifa; na

v. Wananchi.

4.0 HUDUMA ZETU

Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) unatoa huduma kama zifuatavyo:

i. Matengenezo ya vyombo vya moto (magari, pikipiki na Mitambo);

ii. Usimikaji na Utengenezo ya mifumo ya umeme, TEHAMA vifaa vya elektroniki, viyoyozi, majokofu na mitambo;

iii. Ukodishaji wa Mitambo ya kuzalisha kokoto na ujenzi;

iv. Usanifu Mifumo ya mitambo, umeme na elektroniki;

v. Ushauri wa Kitaalam wa mitambo, umeme na elektroniki;

vi. Uzalishaji wa nguzo za taa za barabarani;

vii. Kutathmini kiasi cha Mahitaji ya Umeme (Load study) katika Majengo;

viii. Elimu kwa Umma kuhusu usalama wa vivuko na utunzaji wa magari ya Serikali;

ix. Uvushaji wa abiria, magari, mitambo, vifaa vya ujenzi, mizigo na mifugo kwa kutumia vivuko ‘ferries kwenye maeneo ya Bahari, ziwa na mito;

x. Kufanya mapitio na uhakiki wa michoro ya mifumo ya umeme , elektroniki, lift, mitambo na majengo; na

xi. Huduma nyinginezo.

5.0 VIWANGO VYA HUDUMA ZETU

i. Matengenezo ya vyombo vya moto (magari, pikipiki na Mitambo ya Serikali)

Tutatengeneza vyombo vya moto baada ya makubaliano kwa kuzingatia viwango vya huduma vifuatavyo: -

HUDUMA		MUDA
Matengenezo ya Pikipiki	• Ukaguzi	Ndani ya dakika 30
	• Matengenezo ya kinga	Ndani ya Saa 1
	• Matengenezo ya kawaida	Ndani ya Saa 1
	• Matengenezo makubwa	Ndani ya Saa 2
Matengenezo ya Magari	• Ukaguzi	Ndani ya Saa 1
	• Matengenezo ya kinga (service)	Ndani ya Saa 2
	Matengenezo ya kawaida ya gari	
	• Station Wagon (V8)'	Ndani ya Saa 3
	• Station Wagon (Standard)'	Ndani ya Saa 3
	• Pick up'	Ndani ya Saa 3
	• Saloon car'	Ndani ya Saa 3

HUDUMA		MUDA
	• Bus & Trucks’	Ndani ya Saa 5
	• Mini bus’	Ndani ya Saa 4
	Matengenezo makubwa ya gari	
	Matengenezo ya injini	Ndani ya siku 8
	Matengenezo ya *“geabox”*	Ndani ya siku 3
	Matengenezo ya “Differential”	Ndani ya saa 8
	Matengenezo ya magari yaliyopata ajali (inategemea kiasi cha uharibifu) -	Ndani ya siku 20
Matengenezo ya Mitambo	Ukaguzi wa gari	Ndani ya Saa 10
	Matengenezo ya kinga (service)	Ndani ya Siku 1
	Matengenezo ya kawaida	Ndani ya Siku 3
	Matengenezo ya injini	Ndani ya Siku 7
	Matengenezo ya “Transmission”	Ndani ya Siku 3
	Matengenezo ya “final drive”	Ndani ya Siku 6

ii. Kusimika mifumo ya Umeme, TEHAMA vifaa vya elektroniki, viyoyozi, majokofu na mitambo

a) Kazi za miradi tutasimika mifumo ya Umeme, TEHAMA vifaa vya elektroniki, viyoyozi, majokofu, mitambo, taa za barabarani (Street lights) na taa za kuongoza magari na watembea kwa miguu (Traffic Lights) katika mradi kama itakavyokuwa imelekezwa katika Mkataba wa mradi husika;

b) Kwa kazi za matengenezo na matengenezo kinga tutatengeneza mifumo ya Umeme, TEHAMA vifaa vya elektroniki, viyoyozi, majokofu, mitambo, taa za barabarani (Street lghts) na taa za kuongoza magari na watembea kwa miguu (Traffic Lights) kwa siku zitakazoendana na gharama za kazi kama inavyonekana kwenye jedwali hapa chini;

Na	Kazi kwa kiasi chake kuanzia	Idadi ya siku
1	Tsh. 0.00 mpaka Tsh. 9,999,999.00	Ndani ya siku 7
2	Tsh. 10,000,000.00 mpaka Tsh 19,999.999.00	Ndani ya siku 15
3	Tsh. 20,000,000.00 mpaka Tsh 29,999,999.00	Ndani ya siku 22
4	Tsh 30,000,000.00 mpaka Tsh 39,999,999.00	Ndani ya siku 30
5	Tsh 40,000,000.00 mpaka Tsh 49,999,999.00	Ndani ya siku 40
6	Tsh 50,000,000.00 na kuendelea	Kama itakavyoanishwa kwenye mkataba.

iii. Tutazalisha nguzo za taa za barabarani ndani ya siku nane (8) baada ya kupokea maombi;

iv. Tuna kodisha mitambo ya kuzalisha kokoto na ujenzi ndani ya siku 3 za kazi.

v. Tutavusha abiria, magari, mitambo, vifaa vya ujenzi, mizigo na mifugo kwenye vivuko kwa kuzingatia viwango vifuatavyo: -

A.	Kivuko	Eneo	Muda wa Huduma	Upatikanaji wa Huduma
1.	MV Magogoni	Dar Es Salaam (Magogoni – Kigamboni)	Saa 24	Muda wa asubuhi hadi saa sita usiku Kila baada ya saa 1 kuanzia saa sita usiku
2.	MV Kigamboni			
3.	MV Kazi			
4.	MV Misungwi	Mwanza (Kigongo-Busisi)	Saa 24 Kila baada ya dakika 45	Siku 7 Mara 12 kwa siku
5.	MV Sengerema			
6.	MV Sabasaba			
7.	MV Mwanza			
8.	MV Kome II	Mwanza (Nyakaliro – Kome)	Kila baada ya saa 2	Mara 5 kwa siku
9.	MV Nyerere	Mwanza (Bugolora – Ukara)	Kila baada ya saa 2	Mara 3 kwa siku Siku 7
10.	MV Ukara I & II			

Tanzania Electrical Mechanical and Electronics Services Agency
TEMESA
Wakala wa Ufundi na Umeme
Quality Services for Development Opportunities

A.	Kivuko	Eneo	Muda wa Huduma	Upatikanaji wa Huduma
11.	MV Ujenzi	Mwanza (Kisorya – Rugezi)	Kila baada ya saa 2	Siku 7
12.	MV Chato II	Geita (Chato)	-	Mara 4 kwa wiki
13.	MV TEMESA	Mwanza	Kila baada ya saa 3	Mara 3 kwa siku
14.	MV Tegemeo	Mwanza (Kahunda Maisome)	Kila baada ya saa 4	Mara 2 kwa siku
15.	MV Malagarasi	Kigoma (Ilagala)	Saa 12	Masaa 13 kwa siku
16.	MV Ruvuvu	Kagera (Mto Ruvuvu)	Kila baada ya dakika 5	Mara 10 kwa siku
17.	MV Kyanyabasa	Kagera (Kyanyabasa)	Kila baada ya dakika 5	
18.	MV Musoma	Mara (Musoma – Kinesi)	Kila baada ya saa 2	Mara 5 kwa siku
19.	MV Mara	Mara (Iramba – Majita)	Kila baada ya saa 2	Siku 7
20.	MV Kilambo	Mtwara (Kilambo)	12:30 Asubuhi-2:00 Usiku	Mara 2 kwa siku
21.	MV Mafanikio	Mtwara (Msanga Mkuu)		Kila baada ya saa 1

A.	Kivuko	Eneo	Muda wa Huduma	Upatikanaji wa Huduma
22.	MV Tanga	Tanga (Pangani)	12:00 Asubuhi-4:00 Usiku	Kila siku baada ya nusu saa
23.	MV Pangani II			
24.	MV Mkongo	Pwani (Utete)	Saa 12	Kila siku baada ya saa moja.
25.	MV Kitunda	Lindi (Lindi – Kitunda)	12:30 Asubuhi-1:00 Usiku	Kila siku baada ya nusu saa
26.	MV Ilemela	Mwanza (Kayenze – BEZI – Rugezi – Bukimwi)	Saa 12	Mara 1 kwa siku
27.	MV Kilindoni	Pwani (Nyamisati – Mafia)	Masaa 4	Siku 4 kwa wiki
28.	MV Kilombero 1 & II	Morogoro (Mrimba-kikove) (Malinyi-Ngohelanga)	12:30 asubuhi-1:00 usiku	Siku 7 kwa wiki

vi. Tutasanifu Mifumo mbalimbali kwa kuzingatia viwango vya huduma vifuatavyo baada ya kupata maombi: -

Huduma		**Muda**
Usanifu wa Umeme	Mita za mraba 0-300	Ndani ya siku 40
	Mita za mraba 301-3000	Ndani ya siku 60
	Mita za mraba zaidi ya 3001	Ndani ya siku 100
Usanifu wa Lift zenye Uwezo wa kubeba watu	Watu kuanzia 0-5	Ndani ya siku 38
	Watu kuanzia 5-8	Ndani ya siku 56
	Watu kuanzia 8-24	Ndani ya siku 87
Usanifu wa Majokofu Ukubwa mita za mraba	Mita za mraba 0 - 10	Ndani ya siku 37
	Mita za mraba 11 - 20	Ndani ya siku 64
	Mita za mraba zaidi ya 20	Ndani ya siku 94
Usanifu wa Viyoyozi Ukubwa mita za mraba	Mita za mraba 0 - 300	Ndani ya siku 42
	Mita za mraba 301 - 3000	Ndani ya siku 80
	Mita za mraba zaidi ya 3001	Ndani ya siku 100
Teknolojia habari na mawasiliano Ukubwa mita za mraba	Mita za mraba 0-300	Ndani ya siku 38
	Mita za mraba 301 - 3000	Ndani ya siku 54
	Mita za mraba	Ndani ya siku 94

	zaidi ya 3001	
Utambuzi na tahadhari za majanga ya moto Ukubwa mita za mraba	Mita za mraba 0-300	Ndani ya siku 40
	Mita za mraba 301-3000	Ndani ya siku 54
	Mita za mraba Zaidi ya 3001	Ndani ya siku 94
Kupambana na moto Ukubwa mita za mraba	Mita za mraba 0-300	Ndani ya siku 38
	Mita za mraba 301-3000	Ndani ya siku 54
	Mita za mraba zaidi ya 3001	Ndani ya siku 92

vii. Ushauri wa Kitaalamu katika Fani za Uhandisi Mitambo, Umeme na Elektroniki

a) Tutatoa Ushauri wa Kitaalamu katika Fani za Uhandisi wa mitambo **ndani ya siku tisa (9);**

b) Tutatoa Ushauri wa Kitaalamu katika Fani za Uhandisi wa Umeme **ndani ya siku nane (8)**; na

c) Tutatoa Ushauri wa Kitaalamu katika Fani za Uhandisi wa Elektroniki **ndani ya siku 12.**

viii. Tathmini ya Mitambo, Magari na Vifaa vya Umeme na Elektroniki

a) Tutatoa tathmini ya pikipiki **ndani ya dakika 90 baada ya ukaguzi;**

b) Tutatoa tathmini ya gari **ndani ya masaa mawili (2) baada ya ukaguzi;**

c) Tutatoa tathmini ya Mitambo **ndani ya masaa matatu (3) baada ya ukaguzi;**

d) Tutatoa tathmini ya Magari **ndani ya masaa mawili (2) baada ya ukaguzi;**

e) Tutatoa tathmini ya Vifaa vya Umeme **ndani ya saa moja (1);** na

f) Tutatoa tathmini ya Vifaa vya Elektroniki **ndani ya saa moja (1).**

ix. Tutafanya mapitio na uhakiki wa michoro ya mifumo ya umeme , elektroniki, lift, mitambo na majengo kwa kuzingatia viwango vifuatavyo:-

Huduma		**Muda wa kutoa**
Umeme Ukubwa mita za mraba	Mita za mraba 0-300	Ndani ya siku 3
	Mita za mraba 301-3000	Ndani ya siku 3
	Mita za mraba zaidi ya 3001	Ndani ya siku 10
Lift zenye Uwezo wa kubeba watu	Watu kuanzia 0-5	Ndani ya siku 1
	Watu kuanzia 5-8	Ndani ya siku 3
	Watu kuanzia 8-24	Ndani ya siku 5
Majokofu Ukubwa mita za mraba	Mita za mraba 0 - 10	Ndani ya siku 2
	Mita za mraba 11 - 20	Ndani ya siku 3
	Mita za mraba zaidi ya 20	Ndani ya siku 7
Viyoyozi Ukubwa mita za mraba	Mita za mraba 0 - 300	Ndani ya siku 2
	Mita za mraba 301 - 3000	Ndani ya siku 3
	Mita za mraba zaidi ya 3001	Ndani ya siku 7
Teknolojia habari na mawasiliano Ukubwa mita za	Mita za mraba 0-300	Ndani ya siku 2
	Mita za mraba	Ndani ya

mraba	301 - 3000	siku 3
	Mita za mraba zaidi ya 3001	Ndani ya siku 7
Utambuzi na tahadhari za majanga ya moto Ukubwa mita za mraba	Mita za mraba 0-300	Ndani ya siku 2
	Mita za mraba 301-3000	Ndani ya siku 3
	Mita za mraba Zaidi ya 3001	Ndani ya siku 7
Kupambana na moto Ukubwa mita za mraba	Mita za mraba 0-300	Ndani ya siku 2
	Mita za mraba 301-3000	Ndani ya siku 3
	Mita za mraba zaidi ya 3001	Ndani ya siku 7

x. Tutafanya Tathmini ya Kiasi cha Mahitaji ya Umeme (Load study) katika Majengo kwa kuzingatia viwango vya huduma vifuatavyo:-

Huduma		**Muda wa kutoa**
Umeme	Mita za mraba 0-300	Ndani ya siku 2
	Mita za mraba 301-3000	Ndani ya siku 3
	Mita za mraba zaidi ya 3001	Ndani ya siku 5

xi. Huduma nyinginezo

i. Matangazo yote ya zabuni yatatolewa kupitia mfumo wa ununuzi wa umma (NEST);

ii. Matokeo ya maombi ya zabuni yatafanyika kwenye mfumo wa ununuzi wa umma (NEST);

iii. Tutatoa mikataba ya vifaa/huduma kwa mzabuni aliyeshinda **ndani ya siku 14** za kazi baada ya rasimu ya mkataba kufanyiwa upekusi;

iv. Taarifa za utendaji kazi **ndani ya siku 30** kila baada ya mwisho wa robo mwaka;

v. Tutalipa watoa huduma **ndani ya siku 90** za kazi baada ya kupokea hati ya madai iliyokamilika Pamoja na taasisi iliyohudumiwa kulipa;

vi. Tutatoa mrejesho wa malalamiko ya mteja katika kipindi **ndani ya siku saba (7)** za kazi;

vii. Tutapokea simu za wateja **ndani ya miito mitatu (3**);

viii. Tutakiri kupokea barua **ndani ya siku mbili (2)** za kazi

ix. Tutajibu barua zinazohitaji ufafanuzi **ndani ya siku saba (7)** za kazi baada ya barua kupokelewa;

x. Tutajibu hoja za ukaguzi na kuziwasilisha kwenye mamlaka husika **ndani ya siku 21** baada ya kuzipokea.

6.0 WAJIBU WA WAKALA KWA MTEJA

Ili tuweze kutoa huduma bora zinazokidhi mahitaji ya wateja wetu, tuna wajibu ufuatao:

i. Kutoa huduma zinazozingatia viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa;

ii. Kutoa huduma kwa uwazi na bila upendeleo;

iii. Kupokea ushauri na mapendekezo mbalimbali yenye lengo la kuboresha huduma zetu;

iv. Kupokea malalamiko ya mteja na na kutoa mrejesho;

v. Kutokutoa ama kutokupokea rushwa;

vi. Kuweka taratibu za utoaji huduma zilizo nyepesi na rahisi kwa watumiaji;

vii. Kutoa huduma inayolingana na thamani ya fedha iliyotolewa na mteja; na

viii. Kuwajali wateja, kuwasikiliza na kuwaheshimu.

7.0 HAKI NA WAJIBU WA MTEJA

7.1 *Haki za Mteja*

i. Kupewa taarifa sahihi na kwa wakati;

ii. Kutoa maoni/malalamiko pale ambapo huduma zetu hazikufikia matarajio yake;

iii. Kukata rufaa ikiwa hajaridhika na huduma zinazotolewa;

iv. Kupewa mrejesho kuhusu huduma aliyoomba;

v. Kuheshimiwa na kusikilizwa;

vi. Kutunziwa siri juu ya taarifa zake; na

vii. Kupata stakabadhi halali na sahihi kwa malipo aliyotoa.

7.2 Wajibu wa mteja

i. Kufanya malipo stahili, kwa muda muafaka kulingana na huduma aliyopewa;

ii. Kutunza na kuhifadhi mazingira katika maeneo wanapopata huduma za wakala;

iii. Kutunza siri kadiri ya makubaliano na Wakala isipokuwa kwa mujibu wa sheria;

iv. Kuwaheshimu watoa huduma wa Wakala;

v. kuzingatia Sheria, kanuni na taratibu zinazoongoza utoaji wa huduma husika;

vi. Kutokutoa ama kutokupokea rushwa;

vii. Kutoa taarifa sahihi pale unapotakiwa kufanya hivyo; na

viii. Kuhudhuria vikao na kujali muda kama kuna miadi.

8.0 MREJESHO WA UTOAJI WA HUDUMA

Ili kuhakikisha kuwa wewe mteja wetu unapata huduma bora, tunakaribisha mrejesho kwa njia ya maoni, ushauri, mapendekezo, pongezi au malalamiko. Mrejesho wako unaweza kutolewa kwa njia ya barua, tovuti, barua pepe,

kujaza fomu za tathmini, simu na ana kwa ana kwa kuonana na watoa huduma wetu.

9.0 MAWASILIANO NA TAASISI

Makao Makuu ya Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania yapo katika Jiji la Dodoma, 2 Mtaa wa TEMESA. Wakala una Ofisi za Mikoa na Vituo vinavyojitegemea. Ofisi zetu zitakuwa wazi kuanzia **Jumatatu hadi Ijumaa** saa **01:30 asubuhi mpaka saa 10:30 jioni, Isipokuwa siku za J'mosi, J'pili na siku za Sikukuu za Kitaifa.**Mawasiliano na Wakala yafanyike kwa kutumia anuani zifuatazo:-

Mtendaji Mkuu,
Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA),
TEMESA HOUSE,
2 Mtaa wa TEMESA, 41104 Tambukareli,
S.L.P 1075,
DODOMA.

Simu: +255 737962496
Simu ya bure: 0800110379 Barua
Pepe: barua@temesa.go.tz

Mawasiliano na Ofisi za Mikoa na Vituo vinavyojitegemea

S/N	Mkoa	Barua Pepe	Simu	Sanduku
1.	ARUSHA	rm.arusha@temesa.go.tz	027-2506636	11760
2.	CORPORATION SOLE	m.corpsole@temesa.go.tz	0714184555	1232
3.	DODOMA	rm.dodoma@temesa.go.tz	026-2321866	902
4.	DAR ES SALAAM	rm.dsm@temesa.go.tz	0713225581	75407
5.	MARA	rm.mara@temesa.go.tz	028-600009	81
6.	IRINGA	rm.iringa@temesa.go.tz	026-2702121	228
7.	KAGERA	rm.kagera@temesa.go.tz	028-2221847	733
8.	KATAVI	rm.katavi@temesa.go.tz	0756231286	717
9.	KIGOMA	rm.kigoma@temesa.go.tz	028-2802472	1163

S/N	Mkoa	Barua Pepe	Simu	Sanduku
10.	KILIMANJARO	rm.kilimanjaro@temesa.go.tz	0688483714	3051
11.	LINDI	rm.lindi@temesa.go.tz	0713608924	1022
12.	MANYARA	rm.manyara@temesa.go.tz	027-2530540	264
13.	GEITA	rm.geita@temesa.go.tz	0713266401	619
14.	MBEYA	rm.mbeya@temesa.go.tz	025-2502713	1782
15.	MOROGORO	rm.morogoro@temesa.go.tz	023-2603684	214
16.	MTWARA	rm.mtwara@temesa.go.tz	023-2333909	521
17.	MWANZA	rm.mwanza@temesa.go.tz	028-25022002	691
18.	NJOMBE	rm.njombe@temesa.go.tz	0758759953	1005
19.	PWANI	rm.pwani@temesa.go.tz	023-240258	30150
20.	RUKWA	rm.rukwa@temesa.go.tz	025-2802898	4

S/N	Mkoa	Barua Pepe	Simu	Sanduku
21.	RUVUMA	rm.ruvuma@temesa.go.tz	025-2602179	31
22.	SHINYANGA	rm.shinyanga@temesa.go.tz	028-2762089	62
23.	SIMIYU	rm.simiyu@temesa.go.tz	0757125601	424
24.	SINGIDA	rm.singida@temesa.go.tz	026-2502513	585
25.	TABORA	rm.tabora@temesa.go.tz	026-2604136	804
26.	TANGA	rm.tanga@temesa.go.tz	027-2644080	5678
27.	SONGWE	rm.songwe@temesa.go.tz	0685005896	318
28.	CONSULTANCY	m.kahama@temesa.go.tz	0713413859	2418

I. VITUO VYA FERRY

NA.	Kivuko	Eneo	Mawasiliano
1.	MV Magogoni	Dar Es Salaam (Magogoni – Kigamboni)	0713740840/0624092317
2.	MV Kigamboni		
3.	MV Kazi		
4.	MV Kilambo	Mtwara (Kilambo- Namoto)	0752577655
5.	MV Mafanikio	Mtwara (Msanga mkuu-Msemo)	0756247072
6.	MV Tanga	Tanga (Pangani)	0687836017
7.	MV Pangani II		
8.	MV Mkongo	Pwani (Utete- Mkongo)	0625 811 615
9.	MV Kitunda	Lindi (Lindi – Kitunda)	0718409020

NA.	Kivuko	Eneo	Mawasiliano
10.	MV Kilindoni	Pwani (Nyamisati – Mafia)	0761 371 796
11.	MV Kilombero II	Morogoro (Mlimba-malinyi)	0713257131
12.	MV Ruhuhu	Mbeya (Mwaya-Kajunjumele)	0713257131
13.	MV Misungwi	Mwanza (Kigongo-Busisi)	0715182021
14.	MV Sengerema		
15.	MV Mwanza		
16.	MV Kome II	Mwanza (Nyakaliro – Kome)	0775935764
17.	MV Sabasaba		
18.	MV Nyerere	Mwanza (Bugolora – Ukara)	0754487096
19.	MV Ukara I		

Tanzania Electrical, Mechanical and Electronics Services Agency
TEMESA
Wakala wa Ufundi na Umeme
Quality Services for Development Opportunities

NA.	Kivuko	Eneo	Mawasiliano
20.	MV Ukara II		
21.	MV Ujenzi	Mwanza (Kisorya – Rugezi)	0684972190
22.	MV Chato I	Geita (Chato- Nkome, Chato- Muharamba)	0759952565
23.	MV Chato II		
24.	MV TEMESA	Mwanza (Ilunda- Luchelele)	0613672873
25.	MV Tegemeo	Geita (Kahunda-Maisome- Nkome)	0622018005
26.	MV Malagarasi	Kigoma (Ilagala- Kajeje)	0747151515
27.	MV Ruvuvu	Kagera (Rusumo- Nyakiziba)	0756217188
28.	MV Kyanyabasa	Kagera (Kasharu-Buganguzi)	0765977306

NA.	Kivuko	Eneo	Mawasiliano
29.	MV Musoma	Mara (Musoma – Kinesi)	0765279717
30.	MV Mara	Mara (Iramba – Majita)	0753875994
31.	MV Ilemela	Mwanza (Bezi-Kayenze-Bukimwi)	0625810993
32.	MV Old Ruvuvu	Kagera (Mayenzi-Kanyinya)	0766744344

II. MENEJA WA KANDA

Kanda	Sanduku	Simu	Barua pepe
Meneja wa Vivuko kanda ya Mashariki na Kusini	70704 Dsm	0713257131	m.feszone@temesa.go.tz
Meneja wa Vivuko Kanda ya Ziwa	691 Mwanza	0766744344	m.flakezone@temesa.go.tz

WAKALA WA UFUNDI NA UMEME TANZANIA (TEMESA)
TEMESA HOUSE,
2 MTAA WA TEMESA,
41104 TAMBUKARELI,
S.L.P 1075,
DODOMA

Namba za Simu: +255737962496
Namba ya Bure: 0800110379
Whatsapp: +255737962496
Tovuti: temesa.go.tz
Barua Pepe: barua@temesa.go.tz